

SHULE YA SEKONDARI RUBUGA,
S.L.P 980,
KIGOMA.
14/12/2020

MAWASILIANO:
MKUU WA SHULE – 0765609122
MAKAMU MKUU WA SHULE -0767637465

JINA LA MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUBUGA
KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 Shule ya Sekondari Rubuga ipo umbali wa kilometa tano (05) mashariki ya Halmashauri ya manispaa ya kigoma/ujiji. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/1/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2021.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 Sare ya shule

2.1.1 WAVULANA

- a) Shati nyeupe mbili (tetroni) mikono mifupi inayo fika kwenye kiwiko cha mkono.
- b) Viatu vyeusi vya ngozi.
- c) Soksi ndefu nyeusi.
- d) Suruali mbili za rangi ya kijani kibichi (sampuli ya kitambaa iko shuleni)
- e) Sare ya michezo T-shirt nyekundu moja (01) na bukta nyekundu moja (01)

2.1.2 WASICHANA.

- a) Shati nyeupe mbili (tetroni) mikono mifupi inayo fika kwenye kiwiko cha mkono (isiwe modo)
- b) Viatu vyeusi vya ngozi na kisigino kirefu
- c) Soksi ndefu nyeusi.
- d) Sketi mbili, ya kwanza yenye rangi ya kijani kibichi na ya pili yenye rangi nyekundu (sampuli ya kitambaa iko shuleni shona Linda boksi)

- e) Raba kwa ajili ya michezo
- f) Hijab nyeupe (tetroni).
- g) Sare ya michezo: T-shirt moja (01) yenye rangi ya njano sketi moja (01) yenye rangi ya light blue.

2.2 MAHITAJI MUHIMU.

- Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu.
- Chakula cha wanadunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani na matibabu.

2.3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.1 ya mwaka 1995. aidha, inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare za shule wakati wote.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali ya umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Uulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya taifa
- h) Kuwa mjamzito/kupata mamba


- i) Kuoia au kuolewa
- j) Kutoa mamba
- k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

3.0 VIAMBATANISHO VYA FOMU (MUHIMU)

- a) Medical Examination form (ijazwe na kurudishwa shuleni katika hospitali ya serikali tuu)
- b) Nakala moja (01) ya cheti cha kuzaliwa
- c) Fomu ya historia ya mwanafunzi (ijazwe na kurudishwa shuleni)
- d) Fomu ya kujiunga na shule (ijazwe na kurudishwa shuleni)

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



.....
AIDIA KIRILO
MKUU WA SHULE

IKUJIWA SHULE
RUBUGA SEKONDARI
S.L.P. 980
KIGOMA